

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**16 MEI, 2019**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 16 MEI, 2019**

**I. DUA:**

**II. TAARIFA YA SPIKA:**

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**IV. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**239. MHESHIMIWA SABREENA HAMZA SUNGURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kituo cha Afya Ujiji kinahudumia zaidi ya wakazi elfu ishirini (20,000/=) lakini Kituo hicho hakina mashine ya *ultra sound*:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mashine ya *ultra sound* katika Kituo hicho.

## **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

### **240. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJABU (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Sera ya Serikali ya Viwanda kuhusu zao la Chai hairuhusu Wakulima wa Chai kufungua Viwanda wenyewe ili kuiongezea thamani Chai na hivyo kufanya Kampuni ya *East Usambara Tea Co. Ltd (EUTCO)* iliyoko Amani – Muheza kuathirika:-

Je, kwa nini Serikali isiiondoe Sera hiyo ambayo haiendani na Sera ya Viwanda nchini.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **241. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Wananchi wa Tarafa ya Mombo wamekuwa na hitaji la kuwa na Skimu kubwa ya Umwagiliaji katika Bonde la Mto Mkomazi na mara kadhaa Viongozi wa Serikali wamekuwa wakitoa ahadi ya kukamilisha jambo hilo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa umwagiliaji katika Bonde la Mto Mkomazi.

**242. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANNDA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Halmashauri ya Mji wa Kondoa imewasilisha andiko la mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji katika Kijiji cha Mongoroma, Kata ya Serya takribani miaka mitatu sasa; eneo la ekari 3,000 limetengwa kwa ajili ya mradi huo utakaonufaisha takribani Wananchi 12,000:-

Je, ni lini Serikali italeta fedha hizo ili mradi huo uanze.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**243. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza kwa ukamilifu Sera ya Afya ya kutoa huduma za afya bure kwa Wanawake Wajawazito, Watoto chini ya miaka mitano pamoja na Wazee wenye umri zaidi ya miaka sitini;

- (b) Mwaka 2014 Serikali ilianza utaratibu wa kuwapatia Wazee vitambulisho kwa ajili ya matibabu bure kwenye Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali, Je; ni Wilaya ngapi zimekamilisha zoezi hilo muhimu ili kuokoa maisha ya Wazee yanayopotea kwa kukosa huduma za afya.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**DODOMA  
16 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**